Kutoka Kwa Mkristo

na

Ellis Forsman

Kutoka Kwa Mkristo

na

Ellis Forsman

Aprili 10, 2007

Kutoka Kwa Mkristo

(Ujumbe maalum kwa kijana Mkristo)

Utangulizi

Yesu alisema katika Luka 19:10, "*Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea.*" Hakuja kusuluhisha matatizo ya kisiasa ya Israeli. Au kubomoa ukuta wa Rumi, au kuleta maendeleo katika kilimo, biashara, madawa, au elimu, au kwa kitu cho chote kinachofanana na hayo. Alikuja kuwaokoa wanadamu kutoka dhambini.

Nawataka ninyi vijana wa kiume na wa kike kuwa na usikivu wa kipekee kwa ujumbe huu, kwa sababu kama hujawahi kukabiliwa na ugumu wa kiroho katika maisha yako, au umewahi kufikiria changamoto ya imani yako, muda mfupi utakuwa. Kristo anapoteza waumini (hasa wale walio katika umri mdogo) katika ulimwengu ulipotea na unaokufa kwa kiasi kikubwa, na kuna baadhi ya sababu juu ya swala hili.

Kazi ya kuwafikia waliopotea kwa injili ni kubwa kwa sababu ya kutokuwa na mvuto wa wasio wacha Mungu na wafisadi katika jamii yetu inayopita. Hivi vinamkatisha mtu tamaa kuishi maisha ya Kikristo.

Jamii ya leo inasema, "Kama inajisikia vizuri, fanya!", "Nitafanya kile ninachotaka kufanya wakati ninapotaka kukifanya, na siyo wajibu wa mtu mwingine kadiri jinsi inavyonifanya nijisikie vizuri." Na "Ni mwili wangu, naweza kufanya cho chote ninachotaka na mwili wangu." Tabia kama hii ni ya kibinafsi! Ni makusudi (kuchukulia kivingine kwa ujumbe unaotolewa au mamlaka) kufikiri kuwa mara zote ni sawa kufanya kile ambacho mtu anataka kufanya; ni uasi dhidi ya Mungu kwa sababu mwili wetu sio wetu, ni wa Yule aliyeuumba.

Katika Rum. 12:1-2 Paulo aliandika, "*Basi ndugu zangu nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe namna ya duia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza na ukamilifu.*" Tuna jukumu kwa Mungu kuwa na umakini mzuri wa mwili Aliyotupatia.

Wana wa Israeli kwa kurudia hawakusikiliza ujumbe wa Mungu kwao kupitia Musa, wakichagua kuwa ni afadhali kuwasikiliza wengine labda "ni bora na inashawishi" kuliko yeye, na kwa kusudi la kufahamu kuliko Musa, pia walikataa haki ya Mungu.

Katika tukio fulani, wakati wana wa Israeli walipokusanyishwa chini ya mulima mahali ambapo Waamori walipokuwa wanaishi, Mungu aliwaambia waendelee na safari yao katika nyika na wawaache Waamori wenyewe. Kile kinachoitwa "watu werevu" wa Israeli badala ya kwenda na kupigana na Waamori, wakifikiri "Mungu atatusaidia kama alivyofanya kabla", laini walikuwa wamekosea sana. Mungu hakuwa pamoja nao kwa sababu ya kutokutii kwao. Aliwaambia katika Kumb. 1:43, "*Basi niliwaambia msinisikize, bali mliasi amri ya BWANA, mkajikinai na kukwea mlimani.*" Kwa sababu ya hili walishindwa vibaya, "*Na Waamori waliokuwa wakikaa katika mlima huo, waliwatokea juu yenu, wakawafukuza kama wafukuzwao na nyuki, wakawaporomoshea Seiri mpaka Horma. Mkarudi mkalia mbele za BWANA; BWANA asiisikilize sauti yenu, wala hakuelekeza masikio yake kwenu.*" (mistari ya 44-45).

Watu wengi leo wanajikinai kwamba Mungu yu pamoja nao kwa sababu wanatenda mambo yanayofanana nay a kidini ambayo yanaonekana sahihi kwao. Wanaruka na kuimba sifa kwa Mungu wakipunga, wakiinua mikono, bado hawatii kile anachowaambia kufanya, au wanachukulia kile alichowaambia kama si kitu. Wanafanya kosa la kufikiri kwamba ibada ni kwa ajili ya faida zao – chochote kiwafanyacho wajisikie vizuri. Ibada ni tendo la neno; kitu ambacho kinatakiwa kitendewe Mungu – kutoa ukaribu kwake, au kumwabudu na kumpendeza.

Miaka michache iliyopita, Rais John F. Kennedy alisema, "Usiulize kile ambacho nchi yako itakufanyia; uliza kile utakachoifanyia nchi yako." Kile ambacho kinatakiwa kusemwa leo ni, "Usiulize kile ambacho Mungu atakufanyia; uliza kile utakachomfanyia Mungu." Baada ya yote, ni huduma ya ibada. Hii sio kusema kwamba hatupati faida katika huduma ya ibada sisi binafsi, kwa sababu tunafanya. Nguvu zetu za kiroho hurejeshwa kila wakati tunapokutana, hasa tunapo shiriki ushirika wa meza ya Bwana. Lakini shabaha yetu inapaswa iwe katika kutenda kile kinachomsifu Mungu, siyo kinachotupendezesha sisi.

Mungu aliwaambia Waisraeli katika 1 Sam. 15:22, "*… Angalia kutii ni bora kuliko dhabihu, na kusikia kuliko mafuta ya beberu.*" Yesu akasema katika Yoh. 5:30, "*Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe; kama nisikiavyo ndivyo nihukumuvyo; na hukumu yangu ni ya haki, kwa sababu siyatafuti mapenzi yangu mimi, bali mapenzi yake aliyenipeleka.*" Je unasikia alichokisema Yesu? Anafanya kile kinachompendeza Mungu, siyo yak wake. Kinachompendeza Mungu ni huduma yetu ya ibada ndipo tunapofanya sawasawa na anavyosema. Tukifanya kinyume, tunatenda dhambi ya makusudi, kama walivyofanya Waisraeli.

Daudi alisema katika Mith. 16:25, "*Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu; lakini mwisho wake ni njia ya mauti.*" Alijua kwamba kukusudia kitu ili kikubalike na Mungu sehemu ambapo Mungu

alinyamaza ilikuwa ni dhambi kuu. Sala ya Daudi kwamba asije akatenda dhambi ya makusudi imeandikwa katika Zaburi 19:13, "*Umuzuie mtumishi wako asitende mambo ya kiburi, yasinitawale mimi. Ndipo nitakapo kuwa kamili, nami nitakuwa safi, sina kosa lililo kubwa.*"

Petro alisahihishwa na Mungu kwa kukusudia kwamba ilikuwa sahihi kujenga hema la Yesu, Musa, na Eliya. "*Petro akajibu akamwambia Yesu, Bwana ni vizuri sisi kuwapo hapa; ukitaka nitafanya hapa vibanda vitatu, kimoja chako wewe, na kimoja cha Musa, na kimoja cha Eliya. Alipokuwa katika kusema tazama wingu jeupe likawatia uvuli; na tazama sauti ikatoka katika lile wingu ikasea, Huyu ni Mwanangu mpendwa wangu, ninayependezwa naye, msikieni yeye.*" (Mt. 17:4-5)).

Kwa vile kitu kinaonekana kuwa sahihi kwetu sisi, haimanishi kwamba Mungu anaikubali.

Mvuto wa Dunia

Dhambi hutokea katika ulimwengu kuwa kivutio, hasa katika ujana wa leo. Watu wengi wanafahamu dhambi ni nini na kile ambacho si dhambi. Dhambi husongamana kwa sababu ya udhaifu wa mwili. Kuna mahubiri mengi na makala yaliyoletwa yakizungumzia wazo hili la dhambi, na huo siyo shabaha ya makala hii ambayo inaongelea aina ya vitu ambavyo vinaweza, na huweza kuwachanganya vijana leo, na kuwang'oa kutoka kanisani. Kwa urahisi, fuata ushauri wa mtume Paulo kwa kijana Timotheo: "*zikimbie tamaa za ujanani…*" (2 Tim. 2:22).

Mfumo wa Elimu ya Wengi

Tutaanza na mfumo wa elimu ya wengi. Ulimwengu unawaangalia wasomi wao kwamba ni werevu na sahihi katika matamshi yao na mafundisho. Lakini wengi wao wanadhihaki neno la Mungu na kuichukulia kuwa si sahihi. Wanaharibu sayansi ya kweli na badala yake hufundisha sayansi yao ya uongo; wanawafanyia mzaha wale wanaojaribu kushika imani zao za kidini.

Wakati watoto wengi wanapoandikishwa katika shule zetu za kawaida ninatembezwa katika sehemu ya shule na kuona mazingira. Wanapoonyesha maktaba yao niligundua kwamba vitabu vyao vingi vilijawa na somo la mageuko (mabadiliko), lakini kitabu kimoja kidogo tu ndiyo kilikuwa na mtazamo wa uumbaji. Ilikuwa ni kwaida kwangu kwamba watoto hawatapewa mafundisho na habari iyo hiyo iliyofundishwa nilipokuwa shuleni miaka ya 50.

Nilikuwa na wakati mgumu na mwalimu wangu aliyekuwa akinifundisha Baiologia, ambaye maranyingi alimdhihaki Mungu na

Biblia katika darasa lake. Kama mwanafunzi ye yote alichukulia mambo kwa cho chote alichosema wanakuwa ndiyo mifano katika darasa lake lote. Wakati fulani alitoa madai kwamba kama Biblia inasema kweli kwamba mwanamume leo angekuwa na mbavu pungufu kuliko mwanamke kwa sababu Mungu "kwa bahati" alichukua ubavu wa Adamu na kumtengeneza Hawa. Nilijaribu kueleza jinsi ubishi wake ulivyokuwa na dhihaka kwa kusema kwamba ukikata mkia wa panya, vizazi vyake bado vitakuwa na mkia wa kawaida. Kulikuwa na wachache kama mimi ambao alama zao zilikuwa zikipunguzwa kwa sababu ya changamoto niliyotoa dhidi ya fikira kama hizo.

Wakati mmoja wa watoto wangu alipoleta vitabu vyake kutoka shuleni, nilichukua nafasi kukichunguza kitabu chake cha Baiologia. Siku shangaa kukuta kwamba Mungu na dini zilikosolewa katika sura ya kwanza. Mwalimu hataki dini ifundishwe katika madarasa yao, lakini kwa hakika wanasukuma dini yao ya uongo kwamba "hayupo Mungu."

Ushahidi mwingi wa uumbaji uko katika asili na jiolojia, lakini waalimu wengi hukataa, au hawaruhusiwi, kufundihsa somo hili madarasani. Hii inamwacha mwanafunzi na sayansi ya uongo. Paulo katika barua kwa Timotheo aliandika, "*Ee Timotheo, ilinde hiyo amana; ujiepushe na maneno yasiyo ya dini, yasio na maana, na mashindano ya elimu iitwayo elimu kwa uongo;*" (1 Tim. 6:20). Kuna mifano mingi, mingi sana ya sayansi ya uongo inayofundishwa katika shule zetu za wengi.

Vitabu leo vinaonyesha michoro ya awali katika ukuta ikiwaonyesha wanadamu na wanyama pamoja, kama vile dubu, nyumbu, na simba wa milimani; hataivyo wanashindwa kuonyesha kwamba baadhi ya michoro hii pia inajumuisha mnyama aliyepotea miaka mingi iliyopita (dainosera). Hii huondolewa katika vitabu kwa sababu haiwezi kukaa vyema katika mawazo kwamba mnyama huyu alimzidi binadamu na hakuishi kwa wakati huo kama kile kinachoitwa leo chui wa sikuhizi, nyumbu na simba wa milimani.

Aina ya waalimu hawa wako katika viwango tofauti vya shule zetu, hasa katika vyio vyetu. Wanafundisha kwa "Mungu amekufa!" na kusababisha vijana wetu wengi wachanganyikiwe na kuacha kanisa. Ni kweli kwamba Mungu amekufa katika maisha yao, na Mungu anasema kwamba wao ni wajinga. "*Mpumbavu asema katika moyo wake, hakuna Mungu…*" (Zab. 53:1).

Daktari wa familia yangu, miaka mingi iliyopita, kwamba alipokuwa anakwenda chuo aliamini kila kitu alichoambiwa na mwalimu kwamba sayansi inathibitisha kwamba Mungu hayupo. Alafu, alipokuwa akisoma mchoro wa sikio la mwanadamu, alijiambia mwenyewe, "Haiwezekani kwamba sikio la mwanadamu pia lijumuishwe; hii inaonyesha kwamba mchoro huu uliumbwa."

Ninyi vijana – kama ye yote akikufundisha kwa jina la sayansi kwamba hakuna Mungu, ongea na mtu kanisani kwa ajili ya jambo hili. Usiruhusu imani yenu ipeperushwe kwa sababu ya habari ya uongo. Baadhi ya vijana wa kiume na wa kike wanapokabiliwa na habari kama hizi wanashawishika kwamba wale waliokua katika kanisa wamezeeka na hawajui wanachokiongea. Hakika, walilishwa ujumbe ule ule walipokuwa wadogo, na wakaona uongo ndani yake, hivyo wakabaki imara kiroho. Kuna utajiri wa habari za kisayansi zilizopo ambazo hazipatikani katika vitabu vya shule za kawaida ambazo hazipingi neno la Mungu. Itafute! Omba msaada kama unahitaji.

Shughuli za Shuleni

Shughuli za shuleni pia hubana ukuaji wa kiroho kwa vijana wa leo. Kulikuwa na wakati ambapo hakukua na shughuli za shule zilizokuwa zikipangwa siku za juma pili, lakini wakati huo umeshapita kitambo. Zaidi na zaidi ya vijana wetu wanakosa wakati wa huduma ya kanisa kwa sababu ya shughuli kama michezo, maigizo, muziki, nk. Labda unafahamu idadi ya shughuli, pia ambayo inaingiliana na huduma yako kwa Mungu. Haipaswi kuwa shughuli za shule; inaweza kuwa kitu cho chote ambacho mtu hufanya badala ya kwenda kanisani: ukiweka kambi, vua samaki, ukiendesha boti, ukicheza magongo, kulala…

Miaka mingi iliyopita, Ndg. Tom Broadway alinionyesha kitabu chake cha picha. Kilijaa picha na magazeti na zile alizokuwa akicheza magongo kwa wakati ule akiwa shuleni, na chuo hata alipochezea New York Giants (hiyo ilikuwa kabla ya timu hii kuhamia San Francisco). Tom alikuwa ni mchezaji mzuri katika nafasi kadhaa, lakini kwa ujuzi alikuwa akicheza upande wa kushoto. Anaweza akakuadithia hadithi za kuvutia za kucheza na wacheza mpira wa kikapu wakubwa, kama vile Willie Mays.

Tom alilelewa katika kanisa. Alisema kuwa ilimsumbua wakati alipokuwa akicheza mpira wa mikono, kwa sababu kila mara alikuwa anakosa kwenda kanisani. Mwishowe alijiuzulu katika ujuzi wake kwa sababu alisema haina thamani yo yote. Maisha yake ya kiroho yakawa muhimu sana kwake kuliko mpira wa pete.

Kuna wengi leo ambao wana hisi kuwa hawawezi kuwa na uwezo wa kupata elimu ya chuo, hivyo wanajaribu kujiingiza katika kitu fulani (mara nyingi aina fulani ya mchezo) ilikwamba waweze kupata msaada wa kulipia masomo yao. Haipaswi kuwa hivyo. Shughuli hizi kila mara huwa ni kizuizi cha maisha ya Mkristo. Mara nyingi vyuo wanazo chagua ziko kilomita mamia kutoka katika kanisa la karibu, na kwa wakati wanao maliza elimu yao, Bwana ni kitu kilichopo mbali katika akili zao. Wale wanaodhania kuwa wanapaswa kutoa sadaka dini zao wanapinda

kutafuta ujuzi wao wa kidunia ambao wanaweka mkokoteni mbele ya farasi.

Yesu alisema katika Mat. 6:33, "*Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake na hayo yote mtazidishiwa.*" Ameahidi kwamba tukimtafuta kwanza kwamba atatujali. Usiruhusu shughuli hizi zije katikati yako na Bwana; usidhani kwamba unapaswa kujiingiza katika michezo ili upate elimu ya chuo.

Mafundisho ya Uongo ya Ulimwengu wa Kidini

Wahubiri katika ulimwengu wa kidini waliweka chini injili ya Kristo na badala yake wakaleta hadithi za wakati wa kulala, nyimbo za shule ya awali, habari ndogo ndogo, na mchezo wa kisaikolojia, filosofia, matukio ya muda uliopo, na siasa.

Hivi haviwezi kushawishi ulimwengu wa dhambi; hivi haviwezi kuongoa nafsi kwa Kristo.

Wengi wa viongozi wa dini katika ulimwengu leo hawakubali mamlaka ya maandiko kuhusu mpango wa Mungu wa wokovu. Hata mhubiri wa kanisa la Kristo katika tahariri ya kanisa ambayo nililopokea alijisifu kwamba alihubiri mwaka mzima bila kutaja ubatizo mara moja. Hii haifanani na injili ya kwanza iliyofundishwa na Petro ambapo ubatizo ulifundishwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi.

Wengi wanaridhika kuruhusu jamii ivutie injili yao kuliko kuruhusu injili ya Kristo ivujie jamii yao. Hata makanisa ya Kristo yamebadilika mwaka hadi mwaka. Kulikuwa na wakati ambapo makanisa ya Kristo yote yalikutana kama jinsi tunavyokutana. Alafu wakaangukia katika mvuto wa makanisa ya dini za ulimwengu na kugeuza mambo mengi katika ibada ambayo hayakuagizwa katika maandiko.

Nyuma huko katika 1925, Ndg. George Scott, kaka yake babu yangu, alikwenda Rhodesia Kusini (leo hii ni Zambia) katika Afrika na kutengeneza misheni. Yeye, kwa msaada wa wengine, walitafsiri Biblia katika lugha ya kizambia. Walitumia kikombe kimoja katika ushirika wa meza ya Bwana wakati wa ibada yao. Baada ya miaka 20 alirudi katika nchi hii kuitembelea (Marekani) na alisononeka sana kwa kile alichokiona kanisa lilikuwa limebadilika kwa muda mfupi kwamba akarudi Afrika na kukaa hadi alipofariki katika mwaka wa 1955. Makanisa mengi ya Kristo leo yameachana na injili kwanzia hapo.

Sababu moja ambalo vijana wengi leo wanaacha kanisa ni kwamba wanataka kuburudishwa, badala ya kumwabudu Mungu.

Napaswa kulinganisha ujuzi niliyopata wakati nikiudhuria mafunzo ya jioni katika kanisa lingine la jirani ambalo mke wangu, Lynell, na Mimi tulikaribishwa. Baada ya ibada kuanza, watoto wote wa kila umri

walielekezwa kwenda katika madarasa yao, amabapo michoro mingi ilikuwa ikiwasuria. Wakubwa ambao hawakuhusika katika shughuli hizi walibaki katika sehemu yao husika na “walihudumiwa” katika kiwango cha kuunda bendi ya mziki, wanaume waliimba, wakisaidiwa na wanawake. Hakukuwa na vitabu vya nyimbo vilivyokuwepo kwa ajili ya “kusanyiko” kushiriki. Mziki ulikuwa na mvuto “hisia” nyingi na mdundo, lakini andiko kidogo lina thamani.

Muhubiri aliwatembelea wale miongoni mwa washirika waliokaa mbele alipokuwa akiongea, anawagusa na kuwapiga piga mabegani, labda kuwafanya wajisikie “salama zaidi.” Aliongea kwa ujasiri kwa ajili ya waumini ili waishi maisha makuu, akitumia idadi kubwa ya mifano isiyo ya kibiblia. Alitumia mifano miwili tu ya biblia, na kuyaongopea yote.

Katika moja ya vifungu hivi alisoma Ezek. 1:4-6, na kusema kuwa kifungu hiki kinaelezea mnyama ambaye Ezekieli aliona, “*Nikaona na tazama upepo wa dhoruba ulitoka upande wa kaskazini, wingu kubwa sana pamoja na moto, ukifanya duara ya nuru, na mwangaza pande zote, na katikati yake kitu kama rangi ya karahabu, katikati ya moto huo. Kukatokea katikati yake mfano wa viumbe hai nne. Kuonekana kwao kulikuwa hivi; walikuwa na sura ya mwanadamu. Na kila mmoja alikuwa na nyuso nne, na kila mmoja alikuwa na mabawa manne.*” Soma kitabu cha Ezekieli na utaona kuna mengi zaidi katika maelezo ya huyu mnyama.

Kwa burudani ya nyongeza katika ibada yote, mwanamziki akiwa jukwaani alijaribu kuwavutia watazamaji kwa kuchora picha kubwa ya mnyama ikiendana na maandiko yaliyosomwa na mhubiri. Mwanzo wake haukukamilika ukilinganisha na maelezo yote yaliyotolewa na Ezekieli. Mchoraji pia aliweka picha ndogo ya mtu aliyeko katika kona ya chini ya mchoro, ikionyesha Ezekieli akimtazama mnyama.

Mhubiri huyu alidai ya kwamba Ezekieli hakujua kwamba mnyama huyu alikuwa ni yupi, ya kwamba ni kitu kikubwa mambacho kinafaa kuabudiwa, kwamba Ezekieli alianguka chini na kuiabudu. Nikafikiria mwenyewe “kunakitu ambacho hakiko sahihi na picha hii.”

Haraka nikaweka katika kumbukumbu kitabu cha Ezekieli na siku shangazwa kukuta kwamba Ezekieli hakuabudu mnyama huyu. Katika ukweli, sura ya 10 ya kitabu cha Ezekieli inasema kwamba mnyama huyu alikuwa katika maono ya Ezekieli yalikuwa ni makerubi manne. Unafikiria kama Ezekieli angeabudu, Mungu angemfurahia? Kumbuka, Mungu alisema anawivu na akaamuru kwamba Yeye pekee ndiye wa kuabudiwa.

Andiko lingine ambalo mhubiri huyu alitumia halikuwepo katika neno la Mungu. Alidai kwamba Paulo alisema katika barua yake ya

Waefeso (hakuna kifungu wala msitai) kwamba aliomba kwamba waishi maisha makuu. Sikumbuki Paulo akiliombea swala hili, hivyo kwa haraka sana nikasoma kitabu chote cha Efeso na kupata kwamba mhubiri huyu mambo yake ni ya kutunga. Hakika Paulo aliomba kwamba waweze kumfahamu Mungu vyema (Efe. 1:16), lakini siyo vitu ambavyo mhubiri huyu amevitaja.

Lynell akaniambia kwamba hakutaka kuwapo pale. Nami nikamwambia siyo tu kwa si kuwa na furaha, lakini pia nilishikwa na hasira sana kwa sababu mhubiri huyu alikuwa anawadanganya hawa watu. Mistari miwili tu katika hotuba yote, na zilikuwa zina kosolewa. Ni huzuni kwamba hili ndilo swala katika ulimwengu wote wa kidini. Je hawa wahubiri wanaaibu ya injili ya Mungu kulificha katika hotuba yao.

Paulo alisema katika Waru. 1:16, "*Kwa maana siionei haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza na kwa Myunani pia.*" Pia akasema katika 2 Kor. 4:3, "*Lakini ikiwa Injili yetu imesitirika, imesitirika kwa hao wanaopotea.*" Inasitiriwa kwa sababu imekosa katika hotuba yao yote.

Dhamira za hawa wahubiri huchomwa, kwa sababu hawaonekani kwamba wanajali kile wanachokisema na kufanya wanachojali ni kuwa wamepata majibu ya matakwa yao? Je tabia hii ya "mwisho inaonyesha njia" ya kumpendeza Mungu?

Nilipokuwa kijana katika kanisa, nilihudhuria mkutano wa Injili wa Kibaptist pamoja na Ndg. Howard McCay. Wakati wa hotuba mhubiri alifundisha baadhi ya uongo kana kwamba ni kweli mahali ambapo Biblia imenyamaza. Alipokaribisha waliohudhuria mwishoni mwa somo lake akawaambia kila mmoja kufumba macho yake na ye yeto ambaye angependa aombewe kwa Mungu kwa niaba yao wajitokeze kwa kunyoosha mikono yao. Kwa shauku nilifumba macho na kuinamisha kichwa, alafu nikasikia mhubiri anasema, "Mungu ubarikiwe, ndugu!", "Mungu usamehewe, dada!" au kitu kinacho fanana. Alafu baadaye akamalizia kwa kusema, "Sasa kumbuka, nataka kila mmoja aeshimu siri ya kila mmoja na mfumbe macho yenu." Baada ya hapo, Ndg. Howard akaniambia kwamba alikuwa anatazama matamshi ya baraka juu ya watu wake mahali ambapo mikono haikunyooshwa, vivyo akaangalia katika macho ya mhubiri kwa ukakamavu. Uongo wa mhubiri ulijulikana, lakini bado aliendeleza uongo huo. Baada ya ibada kuisha alimkwepa Ndg. Howard. Uongo kama huo uko katika ulimwengu wa kidini.

Injili ni wazi leo; ni wazi, na mara zote imekuwa uwezo wa Mungu wa kuokoa. Haiwezi kuokoa kama haija hubiriwa! "*Uwatakase na kweli yako; neno lako ndilo kweli.*" (Yoh. 17:17). "*Mkisha kujitakasa roho zenu kwa kuitii kweli, hata kuufikilia upendano wa ndugu usio na unafiki, basi*

jitahidini kupendana kwa moyo. Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika; kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele." (1 Pet. 1 22-23).

Kwa nini watu wengi wanakubali dini ya maji yaliyo machache? Kwa sababu wanataka dhamira isiyosumbuliwa; hivyo hawafanyi uchunguzi katika kile wanachofundishwa. Ama wanaijua, au hapana, kwa makusudi hawamatii Mungu na injili yake, na mara watapotea kama wasipobadilika. "*Na kuwalipa ninyi mteswao raha pamoja na sisi; wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu.*" (2 Thes.1: 7-8). "*Na katika madanganyo yote ya udhalimu kwa hao wanaopotea; kwa sababu hawakukubali kuipenda ile kweli, wapate kuokolewa.*" (2 Thes. 2:10).

Ni aibu kwamba wengi wanapenda kusikiliza ujumbe rahisi, ambao hauna hukumu badala ya kusikiliza neno la Mungu. Paulo alimwambia Timotheo (na sisi pia) kuhubiri neno la Mungu, siyo ujumbe mwingine ambao utasikika vizuri masikioni mwao. "*Nakuagiza mbele za Mungu na mbele za Kristo Yesu, atakayewahukumu walio hai na waliokufa; kwa kufunuliwa kwake na kwa ufalme wake; lihubiri neno, uwe tayari akati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho. Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeuza hadithi za uongo.*" (2 Tim. 4:1-4).

Kuwa makini! Kama mtu ye yote wa dini akihubiri kitu chochote na kuliacha neno la Mungu, ni mbwa mwitu aliyevaa ngozi ya kondoo. Haijalishi hata kama inasikika vyema, au inawasukuma watu, huyo mtu siyo mwakilishi halisi wa Mungu.

Nimewahi kusikia wazee waliotutembelea katika kusanyiko, sawa na makusanyiko mengine wakisema, "Sasa, hayo yalikuwa mahubiri mazuri. Hivyo ndivyo injili ilihubiriwa miaka iliyopita!" walisema ilikuwa inaburudisha kusikia mahubiri mazuri ya zamani. Wengi katika ulimwengu wa kidini leo hawajawahi kusikia mahubiri mazuri ya injili.

Mwinjilisti wa Televisheni

Wakati fulani huko nyuma, kijana mmoja niliyemfahamu alikuwa anatazama mwinjilist wa kwenye runinga ambaye kwa uongo aliponya maradhi ya watu kwa kuwagonga katika paji za nyuso zao na kuanguka chini kwenye sakafu baada ya kuingiwa na Roho Mtakatifu. Kijana

mdogo akaniuliza, “Kwa nini na sisi tusifanye hivyo”? nikamwambia huo ni uongo mtupu; maandiko hayasemi hivyo. Kitu hiki kilimsumbua. Akasema, “Hakiwezi kikawa cha uongo kama iko katika televisheni ya taifa.” Niko hapa kukwambia kwamba kuna uongo mwingi unaoendelea kwa jina la dini.

Mwinjilist wa kwenye televisheni wakati fulani alisema, “Watu hawa wanapoanguka sakafuni baada ya kuwagonga katika paji zao za uso, wako katika hali nyingine kwa sababu Roho Mtakatifu amewaingia na anafanya kazi katika kuponya miili yao.” Nikamwona mwanamke mmoja katika televisheni akipoteza nywele zake za bandia alipoanguka chini kwenye sakafu. Ilifumuka kutoka katika kichwa chake na kwenda umbali kidogo. Kwa haraka akakichukua na kulivaa tena, alafu akaonyesha dalili za kuwepo katika hali nyingine. Kamera kwa haraka ikammulika mwinjilisti huyo wa televisheni, lakini ilikuwa imechelewa. Uongo huo ulijulikana kwa wote.

Paulo aliandika, “*Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya shetani.*” (1 Tim. 4:1).

Nakumbuka nilisoma jarida la gazeti miaka mingi iliyopita ya mkutano wa injili ya hema huko Texas ulioongozwa na Oral Roberts. Mkutano huo ulitangazwa kama mkutano wa uponyaji. Kwa sababu ya umaarufu wa Oral Roberts, hema hilo lilijaa sana. Ghafla upepo ukavuma (uliomaarufu katika Texas) ukainuka na kung’oa hema lile likawaangukia watu. Baadhi yao wakajeruhia pamoja na mifupa kuvunjika kwa sababu ya kuangukiwa na vyuma vilivyo simamishiwa hema hilo. Gazeti hilo lilitoa hesabu kubwa ya idadi ya watu walipelekwa hosipitalini kwa sababu ya majeraha yao. “Kwa “mkutano wa uponyaji” huu ulikuwa ni ufumbuzi wa macho kwa wengi, kwa sababu Oral Roberts asingeweza kufanya chochote kwa ajali hiyo.

Maandiko yanatuonya: “*Jihadharini na manabii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo, walakini kwa ndani ni mbwa mwitu wakali.*” (Mt. 7:15). “*Wapenzi msiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu; kwa sababu manabii wengi wametokea duniani.*” (1 Yoh. 4:1). “*Kwa maana watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza kama yamkini, hata walio wateule.*”(Mt. 24:24).

Wainjilisti wa kwenye televisheni hawapo katika kazi ya kuponya watu; hawapo katika kazi ya kuponya nafsi; bali wapo katika kazi ya kutengeneza pesa. Wanapata wafuasi wengi (hivyo huchanga sana) kwa kuwadanganya watu kwamba wanaweza kuponywa. Mtu anaweza kusikia ujumbe wao kwanzia pembe hadi pembe kwamba tafadhali

watumieni pesa ili waweze kuendeleza kazi ya Mungu (na hivyo kujaza mifuko yao).

Tito 1:10-11, "*Kwa maana kuna wengi wasiotii, wenye maneno yasiyo na maana , wadanganyaji na hasa wale wa tohara, ambao yapasa wazibwe vinywa vyao. Hao wanapindua watu wa nyumba nzima, wakifundisha yasiyowapasa kwa ajili ya mapato ya aibu.*"

"Kanisa la Kristo linachosha"

Wengine wanaacha kanisa la Kristo kwa sababu wanafikiria kwamba inachosha. Wanasema kwamba kusikiliza neno la Mungu likihubiriwa inachosha. Haiwavutii sana, hivyo wanatafuta sehemu nyingine ili waweze kuburudishwa. Tatizo walilonalo ni ukosefu wa ushirika wa ndani na injili.

Paulo alisema katika Fil. 1:3-5, "*Namshukuru Mungu wangu kila niwakumbukapo, siku zote kila niwaombeapo ninyi nyote nikisema sala zangu kwa furaha, kwa sababu ya ushirika wenu katika kuieneza Injili, tangu siku ile ya kwanza hata leo hii.*" Hakika tukimpenda Mungu, shauku yetu ni kukaa katika neno lake.

Msichana mmoja aliweka kitabu ambacho alimaliza kukisoma chini, kwa sifa kwamba kilikuwa ni kitabu chenye hadithi mbaya ambayo hajawahi kusoma.

Kwa sababu ya muda, akaanza uhusiano na kijana mmoja; na usiku mmoja akamwambia kijana huyo, "Ninakitabu katika maktaba yangu ambacho jina la mwandishi, na hata herusi hufanana na yako. Je hilo si jambo geni?

"Sidhani kuwa ndivyo," alijibu.

"Kwa nini sivyo?" binti akauliza.

"Kwa sababu rahisi, ndiyo niliandika kitabu."

Usiku huo, binti huyo alikaa hadi saa 8 za asubuhi akirudia kusoma kile kitabu. Wakati huo kilionekana kitabu chenye mvuto ambacho hajawahi kukisoma. Kwa nini hivyo? Kitabu kilichoonekana kibaya sasa kilivutia kwa sababu alimfahamu na kumpenda mwandishi.

Hivyo ndivyo mwana wa Mungu anakuta Biblia inavutia kwa sababu ametokea kufahamu na kumpenda mwandishi! Kama unadhani kusoma Biblia ni upumbavu, ni wakati wa kurudisha uhusiano wako na Mungu.

“Kanisa la Kristo ni Ndogo Sana haliwezi kuwa Kanisa la Kweli”

Wengine wanaacha kanisa la Kristo kwa sababu wanadhani kuwa ni ndogo sana kuweza kuwa kanisa la kweli.

Yesu aksema, “*Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao.*” (Mt. 18:20). Ukubwa au udigo wa kanisa siyo muhimu. Kilicho muhimu ni kwamba kusanyiko linampendeza Mungu. Waisraeli walidhani kwamba dhabihu zao zilimpendeza Mungu; hataivyo, hii haikuwa kweli kwa sababu ya kutokutii kwao. Samweli akawaambia, “*…Je! BWANA huzipenda sadaka za kuteketezwa na dhabihu sawasawa na kuitii sauti ya BWANA? Angalia kutii ni bora kuliko dhabihu, na kusikia kuliko mafuta ya beberu.*” (1 Sam. 15:22).

Siyo kila wakati kanisa la Kristo lilikuwa ndogo ki idani. Kwa wakati fulani karibia makanisa yote ya Kristo yaliabudu sawasawa na tunavyoabudu, tukitumia kikombe kimoja pekee.

Inavunja moyo tunapopoteza wenzi wetu wengi. Tunaanza kufikiria, “Tumekosea wapi?” Yesu alionyesha kwamba itakuwa hivyo wakati atakapo kuja. “*Na Mungu je! Hatawapatia haki wateule wake wanaomlilia mchana na usiku, naye ni mvumilivu kwao? Nawaambia atawapatia haki upesi; walakini atakapokuja Mwana wa Adamu, je! Ataiona amani duniani?*” (Luka 18:7-8).

Makanisa makubwa kimsingi hawaangalii swali hili ambalo Yesu anauliza kama kutakuwa na mshirika ye yote atakaye baki Yesu akirudi. Kitabu cha Coffman kinasema kwamba: “…kanisa kwa wakati huo wa mwisho, litambunguzwa hadi katika masalio…”

Ninaamini tunakaribia kufika kuja kwa Kristo kwa mara ya pili. Haijajulikana bado ni lini Kristo atakuja, lakini nitakupa kitu ili ukifikirie.

- Enzi za mababu ulianzia katika 4000 B.C.
- Ahadi ya Mungu kwa Ibrahimu ilikuwa 2000 B.C.
- Siku ya Pentekoste (kanisa lilipoanzishwa) ilikuwa 30 A.D.

Ikiwa miaka 2000 kwa kila kizazi kinashikilia ukweli kwa ajili ya kazazi hiki, Mungu vizuri sana angemtuma Yesu kwa wakati huu au katika uhai wa kizazi kijacho.

Yesu akasema, “*Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba peke yake.* (Mt. 24:36).

Ni kweli kwamba hatujui ni lini Yesu atarudi, lakini tunakifahamu kile ambacho Yesu anakiangaikia kama kutakuwa na mwaminifu aliyebaki ndani ya kanisa atakaporudi.

Wakisema kanisa ni ndogo sana kuweza kuwa kanisa la kweli ni ubishi wa hatari. Hakika, hiyo haimanishi tuache kuwaongoa watu kwa Kristo kwa sababu ya ugumu huu. jukumu letu limefanywa kuwa gumu tofauti na ilivyokuwa katika enzi zilizopita.

Ndoa

Yesu alitoa mfano wa mtu aliyeandaa karamu na akawaalika wengine waungane naye. Udhuru mwingi ulitolewa kwa wale ambao walikataa mwaliko huu. mmoja wao akasema, "*Nimemwoa mwanamke hivyo sita kuja.*" (Luka 14:20). Watu wengi wameoa nje ya kanisa na wakawapa wenza wao shinikizo la kuabudu kwingineko. Kijana mmoja akaniambia kwamba alikuwa anaacha kanisa kwa sababu mke wake amemsisitizia kwamba wanaabudu katika kanisa kubwa mahali ambapo kijana wao atapata elimu nzuri ya kiroho. Alisema mkewe alimshinikiza kwa miaka, na ndoa yake ingekuwa hatarini kama asipomsikiliza. Alisema alijua kwamba alikuwa anafanya makosa na akapenda kuabudu na sisi, lakini hakutaka kumwacha mkewe na mtoto, hivyo akaenda.

Maandiko yanatuambia kwamba mjane Mkristo anapaswa kuoa au kuolewa na mjane mwenzake. "*Mwanamke hufungwa maadamu mumewe yu hai, lakini ikiwa mumewe amefariki, yu huru kuolewa na mtu ye yote amtakaye; katika Bwana tu.*" (1 Kor. 7:39). Je Kristo anaweza kutoa agizo kwa mjane hatarajii ye yote kutii? Mkristo ye yote anapooa au kuolewa anapaswa aolewe au kuoa mkristo mwenzake. Petro alielewa hili aliposema, "*…Hakika natambua ya kuwa Mungu hana upendeleo;*" (Mdo. 10:34).

Nabii Amosi alisema, "*Je watu wawili wanaweza kutembea pamoja, wasipokuwa wamepatana?*" (Amosi 3:3). Mtume Paulo akasema Mkristo (na sisi, pia) hafungamani asiyeamini. "*Msifungiwe nira pamoja na wasioamini, kwa jinsi isivyo sawasawa; kwa maana pata urafiki gani kati ya haki na uasi? Tena pana ushirika gani kati ya nuru na giza?*" (2 Kor. 6:14). Ushirika gani mkubwa ulioko tofauti na ushika wa ndoa? Paulo (pia Kristo) waliamuru kwamba kama Wakristo wanataka kuoa au kuolewa, wanapaswa kuwaoa Wakristo wenza.

Sababu ya Bwana kutoa agizo hilo ni kwa sababu alielewa ugumu uliopo wakati mwanamume na mwanamke wana maoni tofauti kiroho. Imani zao zinapokuwa tofauti, watatembeaje kwa amani? Ni nani anayeamua kanisa ambalo watoto wanapaswa kwenda? Ni nani

anayeamua ambacho watoto watafundishwa? Kwa mfumo huo haiwezekani.

Fikiria mwanamke na mwanamume wanasema wanataka kusafiri pamoja; hataivyo mmoja anaamua kwenda New York na mwingine anataka kwenda kisiwa cha Tampa, Florida. Wanawezaje kuanza safari pamoja wakati kila mtu anakwenda kivyake (njia yake)? Hivyo ndivyo ilivyo kiroho. Kama wanachokiamini ni tofauti, njia pekee ya kuwa na amani ni kwa mmoja wao ajiuzulu kwa kile pande zote wanachokiamini.

Chagua mwenzi wako kwa ufasaa!

Je Biblia inaweza kueleweka?

Leo inadaiwa na baadhi ya waalimu wa dini kwamba ukweli ni kitu kinachofanana, hivyo haiwezi kueleweka. Wanadhani kwamba ni upumbavu kuishi sawasawa na neno la Mungu na kuwaita "waliohalalishwa" wanaojaribu kufuata neno la Mungu.

1 Kor. 1:18-21, "*Kwa sababu neno la msalaba kwao wanaopotea ni upuuzi, bali sisi tunaokolewa ni nguvu ya Mungu. Kwa kuwa imeandikwa, nitaiharibu hekima yao wenye hekima, na akili zao wenye akili nitazikataa. Yu wapi mwenye hekima? Yu wapi mwandishi? Yu wapi mlete hoja wa zamani hizi? Je! Mungu hakuifanya hekima ya dunia kuwa ni upumbavu? Kwa maana katika hekima ya Mungu dunia isipopata kumjua Mungu kwa hekima yake, Mungu alipenda kuwaokoa waaminiyo kwa upuzi wa lile neno linalohubiriwa.*" Kabla Yesu hajapaa kwenda mbinguni, aliongelea tabia hii kwa wale ambao hawakumwelewa, au ambao hawakutaka kumwelewa. "*Mbona hamfahamu hayo niyasemayo? Ni kwa sbabu ninyi hamwezi kulisikia neno langu. Ninyi ni wa baba yenu, Ibilisi, na tamaa za baba yenu ndizo mpendazo kuzitenda. Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo; wala hakusimama katika kweli, kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yeke. Asemapo uongo husema yaliyo yake mwenyewe; kwa sababu yeye ni mwongo na baba wa uongo.*" (Yoh. 8:43-44). Ndiyo kwa sababu hii walitaka kumwua. "*Najua ya kuwa ninyi ni uzao wa Ibrahimu lakini manatafuta kuniua kwa sababu neno langu halimo ndani yenu.*" (Yoh. 8:37).

Kuna tabia leo hii ya vijana wadogo kwenda katika intaneti kutafuta majibu ya maswali yao. Nataka nikuonye kwamba hata ingawa kompiuta inaweza kuwa nzuri sana, kuna uchafu mwingi katika intaneti inayotumia jina la dini. Usiamini kila kitu ukisomacho pale; hakika, ni afadhali ukaembali na mafundisho yote ya dini yanayotokea katika intaneti. Utachanganyikiwa! Badala yake, acha Biblia iwe kiongozi wako.

Kwa nini vijana haw wanakwenda katika Intaneti kwa ajili ya majibu yao ya dini? Mara nyingi ni kwa sababu hawapendi kile anachokisema mhubiri katika somo fulani, hivyo wanatafuta majibu wanayo kubaliana nayo.

Kijana mmoja kabla hajaacha kanisa aliazima kompiuta yangu na alikuwa anatafuta baru pepe za makanisa. Alitaka kuangalia kile ambacho wangeweza kuto. Akasema kwamba inawezekana kwamba tumekosa kitu fulani katika huduma yetu ambayo makanisa mengine wanayo 'ugunduzi". Sehemu ya kuangalia kama kitu fulani kimekosa katika huduma ya ibada yetu ni Biblia, sio makanisa ya kidunia ambayo uruhusu karibia kila kitu kwa jina la dini katika huduma yao ya ibada.

Baada ya kusoma sehemu hii, alfu akataka kuhusisha baadhi ya mambo hayo katika ibada yetu, na akachukia tulipokataa kujihusisha nayo.

Baada ya kuongea na baadhi ya wanafunzi wenzake, akashangaa ni kwa nini hatuwaruhusu wanawake kunena katika ibada na akatafuta katika intanei ili kupata majibu. Akapata kwamba baadhi ya barua pepe hizi zilificha kuhusu wanawake kunyamaza kanisani na kwamba wakaja na maelezo yote ili kuliruhusu swala hili. Sehemu fualani katika kompiuta ilidai kwamba kwa vile mwanamume ni kichwa cha mwanamke, kama akisema kuwa ni sahihi kwa mwanamke huyu kunena, hivyo anamamlaka kufanya hivyo.

Baadhi ya anuani hizi zilimtaja Paulo kama si mtu wa Mungu na pia wakaondoa neno lolote katika Biblia ambalo limesemwa na Paulo kwa sababu aliwachukia wanawake. Wanashindwa kuelewa kwamba kile ambacho Paulo alikifundisha hakikutoka kwake mwenyewe, bali moja kwa moja kwa Yesu Kristo. "*Mtu akijiona ya kuwa ni nabii au mtu wa rohoni, na ayatambue hayo ninayowaandikia, ya kwamba ni maagizo ya Bwana.*" (1 Kor. 14:37).

Kijana huyu pia akachanganyikiwa kuhusu ubatizo baada ya kulisoma katika intaneti. Akafikia hitimisho kwamba imani na ubatizo ni kitu kimoja kwa sababu maandiko yanafundisha kwamba tunaokolewa na vyote; hivy (katika akili yake) ni kitu kimoja. Kuna mambo mengi ambayo Biblia inasema tunaokolewa kwalo. Vyote hufanya kazi pamoja ili kukamilisha wokovu wa mtu. Yesu anaonyesha kwamba imani na ubatizo ni mambo mawili tofauti, siyo kitu kimoja. "*Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.*" (Mk. 16:16). Tunafahamu kwa mfano wa ubatizo wa towashi kwamba maji ni muhimu. "*Wakawa wakiendelea njiani, wakafika mahali penye maji; yule towashi akasema, tazama maji haya, ni nini kinachonizuia nisibatizwe? [Filipo akasema, Ukiamini kwa moyo wako wote inawezekana. Akajibu akanena, naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu.]*

Akaamuru lile gari lisimame; wakatelemka wote wawili majini; Filipo na yule towashi naye ambatiza." (Mdo. 8:36-38). Kama maji ni muhimu kwa ubatizo, ni kwa nini kuamini na ubatizo ziwe kitu kimoja? Maji yanauhusiano gani na kuamini?

Intaneti siyo injili.

Kristo na Kanisa Lake Wamepitwa na Wakati?

Viongozi wa kidini wa dunia wanadai kwamba Biblia haiku sawa leo, kwamba inahitajika "iboreshwe" katika upya na kubadilisha ulimwengu. Hivyo, wanafundisha injili ya jamii. Wanapenda kuitwa majina na kumtazama ye yote anayeishi sawasawa na maandiko kwamba "hajasoma". Wanajiita wao wenyewe kwamba wanafunzi wa Biblia, wakati wanakana neno la Mungu. Wanajipatia wenyewe "majina ya kidini" na wanachukia usipotumia au kuwaita majina haya kama (mkuu, Baba nk), wanakataa ukweli kwamba tunaagizwa kivingine. "*Wala msimwite mtu baba duniani; maana Baba yenu ni mmoja, aliye wa mbinguni.*" (Mat. 23:9).

Baadhi ya viongozi wa dini watajiinua kwa umaarufu wao na kuitimu kwao elimu, lakini hawakubali inapokuja wakati wa kufahamu kile anachokitaka Mungu. Badala yake wanahubiri kile wanachopenda kusikia watu. Paulo alifundisha kuhusu hatari ya kufanya kitu kama hicho. "*Maana sasa ni wanadamu ninaowashawishi, au Mungu? Au nataka kuwapendeza wanadamu? Kama ningekuwa hata sasa nawapendeza wanadamu, singekuwa mtumwa wa Kristo.*" (Gal. 1:10). "*Maana ijapokuwa naihubiri Injili, sina la kujisifia; maana nimewekewa sharti tena ole wangu nisipohubiri Injili.*" (1 Kor. 9:16).

Kwa nini kuna tofauti leo? Yohana alifundisha umuhimu wa neno la Mungu. "*Kila apitaye cheo wala asidumu katika mafundisho ya Kristo, yeye hana Mungu. Yeye adumuye katika mafundisho hayo huyo ana Baba na Mwana pia. Mtu akija kwenu naye haleti mafundisho hayo, msimkaribishe nyumbani mwenu, wala msimpe salamu. Maana yeye ampaye salamu azishiriki kazi zake mbovu.*" (2 Yoh. 1:9-11).

Ulimwengu wa kidini haupendi kusikia neno "mafundisho". Kwao ni neno chafu. Alafu, Yohana alisema tusipodumu katika mafundisho ya Kristo, Mungu hayuko ndani yetu. Paulo aliwaonya ndugu wa Wagalatia kutokukubali kila kitu isipokuwa neno la Mungu. "*…Lakini ijapo kuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe. Kama tulivyotangulia kusema na sasa nasema tena, mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo mliyoipokea na alaniwe.*" (Gal. 1:7-9).

Tunatakiwa kuthibitisha kila kitu tunachosikia kuona kwamba ni maneno ya Mungu, na tulikatae kama siyo. "*Wapenzi msiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu; kwa sababu manabii wengi wa uongo wametokea duniani.*" (1 Yoh. 4:1). Kama haiwezi kukutwa kwenye Biblia, ikatae.

Wakati fulani nilimsikia mhubiri akimwambia mtu fulani ambaye hakukubaliana naye, kwamba alikuwa kwamba alikuwa na elimu ya neno la Mungu hakuna mtu anayeweza kumpinga katika kila kitu anachohubiri. Kitu kama hicho ni udhalimu! Paulo akasema, "*Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli.*" (2 Tim. 2:15).

Wengi husema kwamba kila kanisa likiisha; wote tutakwenda mbinguni, tunasafiri tu katika barabara tofauti. Wamekosea sana! Tunaambiwa katika Efe. 4:4-6, "*Mwili mmoja na Roho mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu. Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja. Mungu mmoja naye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote, na katika yote, na ndani ya yote.*" Tunafundishwa katika Mdo. 4:10-12, "*Jueni ninyi nyote na watu wote wa Israeli ya kuwa kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, ambaye ninyi mlimsulubisha, na Mungu akamfufua katika wafu, kwa jina hilo mtu huyu anasimama ali mzima mbele yenu. Yeye ndiye jiwe lile lililodharauliwa na ninyi waashi nalo limewekwa kuwa jiwe kuu la pembeni. Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana* ***jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu*** *litupasalo sisi kuokolewa kwalo.*"

Inasemwa kwamba makanisa yote ya Wakristo uhudumiwa na Yesu Kristo. Mwandishi hapa anasema, "*Hapana jina jingine chini ya mbingu* ***walilopewa wanadamu***." ; hakusema, "hapana mtu mwingine". Yesu akasema, "*Si kila mtu aniambiaye Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni. Wengi wataniambia siku ile Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu.*" (Mt. 7:21-23).

Kanisa linamilikiwa na Yesu Kristo. Kanisa la kwanza lilivaa jina la Yesu Kristo. "*Salimianeni kwa busu takatifu, makanisa yote ya Kristo yawasalimu.*" (Rum. 16:16).

Kanisa pia linaitwa bibi harusi wa Kristo. "*Enyi waume wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda kanisa, akajitoa kwa ajili yake; ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno; apate kujiletea kanisa tukufu, lisilo na hila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa.*" Efe. 5:25-27). "*Siri hiyo ni kubwa, lakini mimi nanena habari ya Kristo na Kanisa.*" (Efe. 5:32).

Hataivyo, hata kama kanisa linavaa jina la Kristo hakuna girantii kwamba ni bibi harusi wa Kristo. Kanisa ni Bibi harusi wa Kristo na linapaswa kuvaa jina lake, kama jinsi mke na mume walivyokuwa wakifanya tangu mwanzo wa nyakati. "*Mwanamume na mwanamke aliwaumba, akawabariki akawaita **jina lao** Adamu, siku ile walipoumbwa.*" (Mwanz. 5:2).

Baadhi ya makanisa ya kidunia wanajiita wenyewe kanisa la Kristo. Wanavaa jina sahihi, lakini maelezo yao hayafanani na maelezo ya bibi harusi wa Kristo, hivyo wao siyo bibi harusi wake.

Ndugu yangu Evart ana jina la mwisho linalofanana na la kwangu – Forsman. Mke wake Becky pia anatumia jina hilo ilo; hataivyo, hataivyo Becky Forsman anatumia jina sawa na la kwangu, yeye siyo bibi harusi wangu. Haendani na maelezo ya bibi harusi wangu. Ndivyo ilivyo hata katika kanisa. Hata kama linajina sahihi hilo halimfanyi kuwa bibi harusi wa Kristo ikiwa maelezo ya Kibiblia hayaendani.

Hitimisho

Tunajukumu la binafsi kuona kwamba tunafanya mambo ya kumpendeza Mungu na siyo wenyewe. "*Wapenzi nilipokuwa nikifanya bidii sana kuwaandikia habari ya wokovu ambao ni wetu sisi sote, naliona imenilazimu kuwaandikia, ili niwaonye kwamba mwishindanie imani waliokabidhiwa watakatifu mara moja tu.*" (Yuda 1:3). "*Mpate kuwa wana wa Mungu wasio na lawama, wala udanganyifu, wasio na ila kati ya kizazi chenye ukaidi, kilichopotoka; ambao kati ya hao mnaonekana kuwa kama mianga katika ulimwengu, mkiishika neno la uzima; nipate sababu ya kuona fahari katika siku ya Kristo, ya kuwa sikupiga mbio bure wala siku jitaabisha bure.*" (Fil. 2:15-16). "*Basi tukiijua hofu ya Bwana, twawavuta wanadamu, lakini tumedhihirishwa mbele za Mungu. Nami natumaini ya kuwa tumedhihirishwa katika dhamiri zenu pia.*" (2 Kor. 5:11).

Tusije tukakata tamaa wakati juhudi zetu zinaonekana kutuangusha. Kama maneno ya mhubiri wa zamani, "Tunapaswa kujitahidi na kuendelea." "*Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake tusipozimia roho.*" (Gal. 6:9). Kaa katika sababu na uilinde imani.